

Ndugu waheshimiwa, wapendwa wanafunzi na marafiki zetu,

Tunapozindua mwaka mpya ni furaha yetu kubwa kutangaza kikao kifuatacho cha

Baraza letu la Kiswahili la Berlin (BALAKI-BE) la tarehe 08 Januari 2024

**Kuwapo Kwa Mitazamo Tofauti Katika Kuwepo Kwa Maua: Uchambuzi wa Riwaya ya
Kuwa kwa Maua ya William Mkufya**

Cristina Nicolini

Katika wasilisho hili Cristina Nicolini atachambua riwaya ya *Kuwa kwa Maua* iliyoandikwa na mwandishi mtajika William Mkufya na kuchapishwa mwaka 2019. Uchambuzi wake utajikita katika mtazamo wa kiontolojia wa riwaya hii ambapo mwandishi anaendeleza mazungumzo aliyoyaanzisha katika riwaya yake ya *Ziraili na Zirani* (1999). Tofauti na riwaya hiyo, Mkufya amejiepusha kabisa na mada za kimetafizikia na badala yake amewaruhusu wahusika wake kuweka chini silaha zao zilizotengenezwa kwa lengo la kupigana na dini. Badala yake, amezihamishia mapambano hayo ndani ya nafsi za wahusika. Zaidi ya hapo, kwa ukosoaji mkubwa mwandishi anaishia katika mazingira ya amani yanayokubaliana na utofauti. Uchunguzi wa mazingira ya kuwapo katika amani kwa mitazamo mbalimbali unafanyika kwa njia ya falsafa ya udhahiri ambayo inahusu udhaifu wa “maua” – yaani watu wema – wakati wanapojenga utu wa kweli.

Dkt Cristina Nicolini anayo shahada ya uzamifu ya lugha na tamaduni za Kiafrika ya Chuo Kikuu cha SOAS huko London. Tasnifu yake ‘Mgongano wa Ujuzi: Ufahamu wa UKIMWI katika Tazunguzo za Fasihi ya Kiswahili’ ilichapishwa mwaka 2022. Kwa sasa Dkt Nicolini ni mtafiti wa baada ya uzamifu wa shirika la Fritz Thyssen kwenye Idara ya Afrika, Asia na Mediterania ya Chuo Kikuu cha Napoli ‘L’Orientale’.

Kikao kitafanyika **siku ya Jumatatu, tarehe 08 Januari 2024, saa kumi kamili za Ulaya ya Kati** (saa kumi na mbili za Afrika Mashariki) **kupitia njia ya Zoom:**
<https://us02web.zoom.us/j/82239014153?pwd=eG9KbXINdUFJbGkwV243MG9IRjRGdz09>

KARIBUNI NYOTE!

Tafadhalini wajulisheni wapenzi wote wa Kiswahili na marafiki wengine!

Wasalaam,

Kai Kresse, Lutz Diegner na Maxwell Omondi Ondieki

Kama kuna maswali yoyote kuhusu baraza bili tafadhalini mwandikieni mwenzetu:
<MaxwellOmondi.Ondieki@zmo.de >